

- Taarifa ya Idara ya Ardhi na Maliasili- wajumbe waliridhia Taarifa na hapakuwa na masahihisho yaliyofanyika.
- Taarifa ya Idara ya Ujenzi - Wajumbe walipitia taarifa na marekbisho yalifanyika kwenye utangulizi kuwa ioneshe kuwa inawasilishwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi.
- Aidha, ilishauriwa kuwa shughuli za Idara ya Ujenzi zionekane badala ya miradi ya Idara zingine kwa ujumla kama uandaaji wa makadirio ya ujenzi katika miradi mbalimbali, uandaaji wa Michoro na ufuatiliaji wa miradi.

3. Kamati Shirikishi ya kudhibiti UKIMWI (CMAC)

- Wajumbe waliridhia taarifa zilizowasilishwa kuwasilishwa kwa wajumbe wa Kamati Shirikishi ya Kudhibiti UKIMWI (W) na hapakuwa na marekebisho zaidi.

MUHTASARI NA.127/2021 TAARIFA YA MAOMBI YA KUIDHINISHIWA KIASI CHA TSH.27,428,500.00 KWA AJILI YA UFYATUAJI WA MATOFALI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA YA SHULE SHIKIZI, MADARASA YA SEKONDARI NA NYUMBA ZA WATUMISHI WA AFYA (3:1)

- Wajumbe walielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya imetengewa kiasi cha Tsh.2,110,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 57 ya Shule Shikizi, vyumba vya madarasa 44 ya Shule za Sekondari na nyumba za watumishi wa Afya (3:1)
- Wajumbe walielezwa kuwa ujenzi wa majengo hayo utahitaji matofali takriban 255,000 hivyo Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ilijadili na kupendekeza kununuliwa kwa mashine kwa ajili ya mradi wa ufyatuaji wa matofali.
- Ilielezwa kuwa mchanganuo wa maombi haya ni kama ifuatavyo;

Na.	Maelezo ya Shughuli	Gharama (Tsh.)
1.	Kununua mashine 2 @ Tsh.7,000,000.00 za ufyatuaji wa matofali	14,000,000.00
2.	Kununua vifaa na gharama za kuvuta umeme pamoja na kutengeneza vibao 5,000 vya kufyatulia matofali	6,856,500.00
3.	Gharama za kununua vifaa na kuvuta maji kutoka Hospitali ya Wilaya kusafisha Eneo la kufyatulia, kujenga karo la maji na kujenga banda la kufyatulia	6,572,000.00
	Jumla Kuu	27,428,500.00

- Wajumbe waliridhia taarifa na kufuatiwa na mjadala kama ifuatavyo;

Mjadala;

- Wajumbe walikubaliana kuwa katika mradi wa ufyatuaji wa matofali ni vyema vibao vya mbao vitumike badala ya "fibre".
- Wajumbe walishauri kuwa Timu ya Wataalam wafanye ufuatiliaji katika Chuo cha "Arusha Technical" pia CARMATEC na SIDO ili tuweze kupata mashine mapema.
- Wajumbe walishauri kuwa Afisa Maendeleo ya Jamii (W), Afisa Mipango (W), na Mhandisi wa Ujenzi wakae na kuwasilisha mapendekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji juu ya namna bora ya

kutekeleza mradi huu kwa ufanisi na baada ya hapo kikao cha Wakuu wa Idara kitafanyika tarehe 15.10.2021 ili kupata mrejesho wa mapendekezo yaliyofikiwa.

- Wajumbe walishauri kuwa ili kuwe na ufanisi katika zoezi la ufyatuaji wa matofali ni vyema maeneo ya mbali wafyatue matofali wenyewe ili kupunguza gharama na kuokoa muda.
- Wajumbe walishauri kuwa ni vyema fedha za mradi zitakapopokelewa ndipo manunuzi ya saruji yafanyike.
- Wajumbe walishauri kuwa ni vyema nukuu za bei ya saruji ziombwe viwandani mapema ili kuepusha kupanda kwa bei. Ilisisitizwa kuwa ni vyema wahandisi wajitahidi kuhakikisha kuwa makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) zinakuwa ni uhalisia ili kuepusha kununua vifaa vinavyozidi mahitaji halisi.

MUHTASARI NA.128/2021 TAARIFA YA MANUNUZI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI-SEPTEMBA 2021)


- Wajumbe walielezwa kuwa katika kipindi hiki Halmashauri ya Wilaya ilifanya Manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali yenye thamani ya **Tsh.941,624,929.00** kati ya Lengo la kununua bidhaa na huduma mbalimbali zenye thamani ya **Tsh.1,962,500,867.00** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 sawa na asilimia 48 ya lengo.
- Wajumbe waliridhia taarifa na hapakuwa na mjadala zaidi.

MUHTASARI NA.129/2021 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

- Mjumbe alitoa hoja kuwa ni vyema Timu ya Menejimenti igawanyike kwenye kanda ili kuwezesha usimamizi wa miradi yote kuwa na ufanisi.

MUHTASARI NA.130/2021 - KUFUNGA KIKAO

- Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kufanikisha kikao na alisisitiza kuwa maagizo yaakelezwe kwa wakati na baada ya kusema maneno hayo alifunga kikao saa 6:20 mchana.


.....
Bw. John John Nchimbi
Mwenyekiti

UMETHIBITISHWA


.....
Bi. Beatrice Rumbeli
Katibu

Tarehe. 12.11.2021.....

